MWITO PROGRAM

PROG: 1155 KISWAHILI SCRIPT

DURATION:15 MINUTES

MESSAGE:10 MINUTES

SCRIPTURE:ROMANS 8:28

INTRO:

Mpendwa msikilizaji nakualika uwe nami kwa dakika 15 zijazo kwa kipindi hiki ukipendacho cha Mwito.Kipindi hiki ni sehemu ya huduma ya kimataifa yake Mchungaji Harold Williams,kwa jina la Macedonial Call na kimeandaliwa katika studio za Transworld Radio,Nairobi.

Nakukaribisha kwa kipindi cha leo ambacho ni nambari 1155.Ninaamini ulikuwa na wiki njema na sasa uko tayari kwa kipindi hiki.Sina shaka uko na kalamu,bibilia yako pamoja na mahala pa kuandika nasaha kutokana na somo la leo.Naamini umemjulisha rafiki kuhusu kipindi hiki na mnasikiliza pamoja.Kumbuka pia weza kujipatia nakala ya Agano jipya la Bibilia takatifu.Sikiliza hadi mwisho nitakweleza jinsi.

Kwenye kipindi kilichopita tulisoma kutoka aya ***ya 28 ya Warumi sura ya 8….. Nasi twajua kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia meema ,yaani wale walioitwa kwa kusudi lake.***Kwa hakika aya hiyo ina maana kubwa hasa kwa waaminio.Leo kwenye kipindi hiki kipya nambari 1155 tutasoma aya ya 29 ya Warumi sura ya 8.Naomba tusome pamoja….***Maana wale aliowajua tangu asili aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa mwana wake,ili yeye naye awe mzaliwa wa***

kwanza miongoni mwa ndugu wengi.aya ya 30…N a wale aliowachagua tangu asili hao akawaita;na wale aliowaita,hao akawahesabia haki;na wale aliowahesabia haki,hao akawatukuza.

Naam tumeshausoma ule msitari wenye matumani makubwa unaotuhakikishia kuwa yote hutendeka kwa wema kwa wale wampendao Bwana na wale ambao wameitwa kwa kusudi lake.Si hiyo ni ahadi nzuri mpendwa? Wale wampendao Mungu.Wale ambao wameitwa kwa kusudi lake.Hata ingawa huenda wasijue hilo,licha ya kupitia ugumu wa maisha,Mungu atatimiza ahadi yake katika maisha yao.Hata wakifikia kiwango cha kutojua jinsi ya kuomba na hata kile cha kuombea,Mungu atafanya yote kuwa mema mwishoni.Mungu anatenda hayo ndani yetu akituimarisha na kutufanya watauwa kwa ajili ya ufalme wake.Huko ndiko MUngu anatuelekeza.Na sasa tunakuja kwenye kifungu ambacho kidogo kimekanganya baadhi yetu… ***Maana wale aliowajua tangu asili aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa mwana wake,ili yeye naye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi.*** Naam swali ni kwamba,Ni nani aliowajua tangu asili? Swali zuri hilo.Naam kupata jawabu tutarudi nyuma kabisa hadi aya ya kwanza ya sura ya nane ya kitabu cha Warumi.Hiyo aya inasema kwamba..***Sasa basi hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu.Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru,mbali na sheria ya dhambi na mauti.*** Naamini umeupata msitari huo vizuri.Wale walio katika Kristo Yesu ndio wanaozungumziwa tangu mwanzo wa sura hii ya nane ya warumi hadi mwisho.Wale walio katika Yesu Kristo ndio wale aliowajua tangu asili na kuwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa mwana wake,ili yeye naye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi.Maneno hayo..aliyewajua tangu asili….yanamaanisha Mungu alijua kimbele yale yatakayotendeka.Ni kama unabi ambao mwanzo mwanzo huwa kama

historia ilioandikwa kimbele.Mungu aliujua mwisho wa mambo tokea mwanzo.Mungu alijua mpango mzima na utaratibu wote.Wajua nini msikilizaji wangu ,Mungu hata hajishughulishi na hali ya uchumi,ukosefu wa kazi wala mfumko wa bei ya bidhaa.Yaani mambo yote yanayotushughulisha ,hayamsumbui Mungu hata kidogo.Sisi kama binadamu hata hatuwezi kujua yalio ,bele ya kona ya maisha ambayo tutabeta.Lakini mpango wa Mungu ni imara na madhubuti.Hauchelewi hata dakika moja wala kwenda mbele kwa dakika moja.Matukio yake yanajitokeza kwa usambamba jinsi Mungu mwenyewe alivyonuia.Ni kusema kwamba neno la mshangao kama vile ala au kumbe! Hayapo kwenye msamiati wa Mungu.Hakuna linalojiri bila yeye kulijua awali.Anaujua mwanzo kutoka mwisho wa jambo.Nina furaha ya kumtumikia MUngu wa aina hii.Kwa hivyo …. ***basi hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu.***Na wae walio katika Yesu Kristo ndio wale …. ***aliowajua tangu asili na kuwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa mwana wake,ili yeye naye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi***

Maandiko yanaendelea kusema kuwa aliyewajua tangu asili.. ***aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa mwana wake,ili yeye naye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi***

Naomba ufungue nami katika kitabu cha Matendo ya mitume sura ya 2 na aya za 22 hadi 23.Huyu ni mtume Petero siku ya pentekote alipokuwa akiwahubiria makutano hasa wayahudi wasioamini na viongozi wa kidini aliposema…***Enyi waume wa Israeli***…***Yesu wa Nazareti mtu aliyedhihirishwa kwenu na Mungu kwa miujiza Na ajabu na ishara ambazo Mungu alizifanya kwa mkono wake kati yenu kama ninyi wenyewe mnavyojua.Mtu huyu alipotolewa kwa shauri la Mungu lililokusudiwa na kwa kujua kwake tangu zamani ,ninyi mkamsulubisha kwa mikono ya watu***

wabaya ,mkamuuwa;ambaye mungu alimfufua akiuungua uchungu wa mauti kwa saabu haikuwezekana ashikwe nao.

Hapa ndipo mahal pagumu kwa baadhi yetu,ambapo utatu mtakatifu unasemekana ulishauriana yaani Mungu Baa ,MUngu mwana na Mungu Roho mtakatifu mkondo wa mambo tangu kuzaliwa kwa Kristo hadi umauti ulipokumbana naye.Ilibainika kuwa Kristo angeliuawa msalabani kam dhabihu ya dhambi zetu.Hapa MUngu hakuchagua watakaookolewa na ambao hawataokolewa.Aliwapa watu shauku ya kuokoka ,bila kuwalazimu.Tangu mwanzo Mungu alijua wale wtakaookolewa na ambao hawataokolewa.Naomba ndugu msikilizaji kukomea hapo.utendelea kesho na somo hili.Jiunge nami kwa kipindi ijacho cha Mwito.Ikiwa hujaokoka nakupa himizo ufanye hivyo.Tubu dambi zako na umpokee Kristo kuwa mwokozi wako.Jijulishe kwa viongozi wako kanisani ikiwa umefanya uamuzi wa kuokoka. Niandikie ili tuweze kufahamiana zaidi. Nitafurahi sana kuwasiliana nawe na ahata kukupatia vijitabu nan akala ya agano jipya la Bibilia kukusaidia kuweka msingi imara wa ukristo wako. Zaidi ya hayo.Nitafurahi sana nitakapopokea maoni yako kukihusu kipindi hiki na hasa jinsi ya kukifanya kiwe cha manufaa zaidi kwako.Hiki kimekuwa kipindi cha Mwito nambari 1155.Naomba uwasiliane nami kupitia njia ya arafa ukitumia nambari ifwatayo-: 0721 970 520. Au 020 2679842.Ikiwa unaishi Nairobi tunakukaribisha ututembelee kwenye studio zetu za TWR Kamburu Drive,off Ngong Road, baada ya jumba la TOP PLAZA.Anwani yangu ikiwa utaniandikia barua ni-:Kwa mtayarishi,Mwito,S.L.P.21514-00505 Nairobi.Waweza pia kuwasiliana nami kwa njia ya barua pepe ifwatavyo-barua@twr.co.ke.Na basi kufikia hapo sina budi kulikunja jamvi langu kwa leo ninapokutakia baraka sufufu kutoka kwake Mungu wetu mtukuka.Juma lijalo tutaingia aya ya 28 ya sura ya 8 ya kitabu cha Warumi.Ni mwaandazi wa kipindi hiki ndugu Charles Otunga ninayekuaga nikikutakia mbawazi zake Mungu wetu mtukuka.Kwaheri.